

SAUTI YATSC

TOLEO NA. 48 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** FEBRUARI 2025

KAMATI YA BUNGE YATAMANI MAREKEBISHO KATIKA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Justin Lazaro Nyamoga (kushoto) akiongoza kikao cha kamati hiyo tarehe 21 Januari, 2025 ambapo taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 iliwasilishwa. Kulia ni Katibu wa Kamati hiyo Bi. Sikudhani Mbinga.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

MASLAHI YA WALIMU KUWEKWA KIPAUMBELE KATIKA SERA YA ELIMU NI FARAJA KUBWA KWA WALIMU

Siku chache zilizopita Rais Samia Suluhu Hassan amezindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 na kueleza kuwa serikali itapitia upya maslahi ya kada ya walimu ili kuipa hadhi inayostahili kama mama wa taaluma zote duniani.

Alisema kuwa pamoja na uhitaji wa rasilimali na miundombinu ya elimu, kiungo kikubwa katika utekelezaji huo ni mwalimu.

Alisema mwalimu ndiye kiongozi wa elimu, hivyo katika maboresho hayo lazima awe katikati ya mduara wa maboresho.

Aliitaka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuwezesha na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sera hiyo ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Taarifa hiyo ni habari njema kwa walimu na ni ishara njema kuwa changamoto na malalamiko ya walimu kuhusiana na maslahi yao sasa itakuwa historia.

Tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa kutoa kipaumbele katika kuboresha maslahi ya walimu jambo ambalo litasaidia kuongeza kasi ya kujituma, bidii, ufanisi weledi na uzalendo kwa walimu katika utekelezaji wa majukumu yao.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KAMATI YA BUNGE YATAMANI MAREKEBISHO KATIKA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Justin Lazaro Nyamoga (kushoto) akiongoza kikao cha kamati hiyo tarehe 21 Januari, 2025 ambapo taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2024 iliwasilishwa. Kulia ni Katibu wa Kamati hiyo Bi. Sikudhani Mbinga.

Na Mwandishi Wetu-Dodoma

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeshauri kuangaliwa uwezekano wa kufanyia mabadiliko Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 kwa ajili ya kuondoa changamoto zinazokwamisha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Justin Lazaro Nyamoga, ametoa kauli hiyo tarehe 21 Januari, 2025 wakati Kamati hiyo ilipopokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 02 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024.

Mhe. Nyamoga alisema kuwa uboreshaji wa Sheria utaiwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika kutoa huduma bora kwa walimu na hivyo kuinua Sekta ya Elimu nchini.

Aidha, Kamati imeshauri Serikali kuweka mkazo katika utoaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Tume ya Utumishi wa Walimu ili liweze kukamilika kwa wakati kwa ajili ya kuwasaidia watumishi wa Taasisi hiyo kuwa na mazingira mazuri ya kuwahudumia

walimu.

Mwenyekiti wa Kamati aliongeza kuwa sanjari na kuweka mkazo katika ujenzi wa Makao Makuu ya Tume, ni vema ujenzi wa Ofisi za Tume katika kila Wilaya ukaanza ili watumishi wawe na mazingira mazuri ya kuwahudua Walimu.

Kwa upande wake, Naibu Waziri

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Zainab Katimba alisema kuwa Serikali imechukua maelekezo ya Kamati hiyo na itayafanyika kazi.

Awali Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwana akiwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 02 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea na kutumia jumla ya Shilingi 8.5 sawa na asilimia 41 ya kiasi cha Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha wa 2024/25.

Alisema kuwa kati ya fedha hizo shilingi 5.1 ni Mishahara, shilingi bilioni 2.1 ni matumizi Mengineyo (OC) na shilingi bilioni 1.1 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Desemba, 2024, Tume ya Utumishi wa Walimu iliendelea kuhudumia jumla ya Walimu 273,736 wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo kwenye Utumishi wa Umma.

Alisema kuwa kati yao Walimu wa Shule za Msingi ni 180,870 na Sekondari ni Walimu 92,886.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Zainab Katimba akitoa ufafanuzi tarehe 21 Januari, 2025 wakati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walipopokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024.

KAMATI YA BUNGE YATAMANI MAREKEBISHO KATIKA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Zainab Katimba akitoa ufafanuzi tarehe 21 Januari, 2025 wakati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa walipopokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa tarehe 21 Januari, 2025.

Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Tarime Mhe. Mwita Waitara akitoa maoni wakati wa Kamati hiyo ilipokuwa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 jana tarehe 21 Januari, 2025.



Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo La Urambo Mhe. Magreth Sitta akitoa maoni wakati wa Kamati hiyo ilipokuwa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 jana tarehe 21 Januari, 2025.

KAMATI YA BUNGE YATAMANI MAREKEBISHO KATIKA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakifuatilia wasilisho ya Tume ya Utumishi wa Walimu kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 jana tarehe 21 Januari, 2025.



Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakirwa katika kikao cha kurwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 kilichofanyika tarehe 21 Januari, 2025 kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

TSC NANYUMBU YAJIDHATITI KUDHIBITI UTORO, KUKOPA KUPITA KIASI

**Na Mwandishi wetu –
Nanyumbu.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nanyumbu imeendelea na mikakati mbalimbali ili kukabiliana na ukiukwaji wa taratibu za kiutumishi unaofanywa na baadhi ya walimu wachache katika Wilaya hiyo.

Miongoni mwa vitendo vinavyofanywa na baadhi ya walimu hao ni kukopa kupita kiasi kulingana na taratibu za utumishi wa umma pamoja na utoro unaosababishwa na kuondoka katika kituo cha kazi bila kukamilisha taratibu zinazotakiwa.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Afisa wa TSC katika Wilaya Nanyumbu, Bw. Yohana Mrekoni katika mahojiano maalum na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali wa TSC waliotembelea ofisi za Tume katika Wilaya hiyo kwa lengo la kupata habari juu ya namna TSC inavyowahudumia walimu katika Wilaya ya Nanyumbu.

Bw. Mrekoni alieleza kuwa kuna walimu wachache ambao wamejiingiza katika mikopo umiza jambo linalowaondolea utulivu wa kufundisha wanafunzi kwa kuwa mara kwa mara waliowakepesha wanafika shuleni kudai fedha zao huku walimu wakiwa hawana fedha za kulipa.

".....kwa mfano, hivi karibuni tulikuwa na Mwalimu mmoja ambaye kila kampuni inayokopesha hapa Nanyumbu alikopa, baada ya kukopa kampuni zote akahamia



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nanyumbu, Bw. Yohana Mrekoni akitoa ufafanuzi wakati wa mahojiano maalum kati yake na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (TSC) (hawapo pichani) yaliyofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Nanyumbu.

kwenye Kampuni za Wilaya ya Masasi napo akakopa. Baada ya kuona anadaiwa na hana fedha za kulipa akaamua kukimbia na kuacha kazi," alisema Bw. Mrekoni.

Akizungumzia sababu za utoro, Bw. Mrekoni alieleza kuwa wapo baadhi ya walimu ambao wanapata ajira maeneo mengine nje ya utumishi wa umma lakini badala ya kufuata taratibu za kuacha kazi, wanaondoka bila kutoa taarifa na hivyo kufunguliwa mashauri ya nidhamu na mwishowe wanafukuzwa kazi.

"Mtumishi wa Umma hapaswi kuacha kazi tu bila kutoa taarifa na kukamilisha taratibu zote kama inavyohitajika. Lakini huku bado kuna walimu wachache wakishaona wamepata ajira sehemu yenye maslahi zaidi wanaondoka tu bila kutoa taarifa kwa mwajiri. Hata tukiwapigia simu na kuwasihi wafuate taratibu hawataki kusikikiliza," alisema Bw. Mrekoni.

Aliongeza kuwa, "Kibaya zaidi

wapo walimu wanaokwenda kukopa benki, wakiona tu fedha ya mkopo imeingia wanaacha kazi na kwenda kuanzisha biashara zao."

Katika kukabiliana na changamoto ya kutonzingatiwa kwa Kanuni za Maadili ya kazi ya Ualimu, Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutoa elimu kwa walimu kupitia vikao, mikutano, ziara shuleni pamoja na kuongea na mwalimu mmoja mmoja kwa lengo la kutoa nasaha.

"Kwa mwaka jana (2023/2024) tulifanikiwa kufanya mikutano na walimu katika kata 10 kati ya kata 17 za Wilaya ya Nanyumbu. Tunaona kuwa elimu tunayotoa inasaidia walimu kubadilika kitabia. Katika miaka ya hivi karibuni hali ya nidhamu imeendelea kuimarika tofauti na ilivyokuwa huko nyuma, alisema Bw. Mrekoni.

Kwa mujibu wa Afisa huyo, katika Mwaka wa fedha 2021/2022 kulikuwa na mashauri ya nidhamu saba (7), mwaka 2022/2023 kulikuwa na mashauri matano (5), mwaka 2023/2024 mashauri 4 na katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, 2025 hakuna shauri lolote lililofunguliwa.

Wilaya ya Nanyumbu ina jumla ya walimu 882 wanaohudumiwa na TSC, kati ya hao walimu 610 ni wa shule za msingi na 272 ni wa shule za Sekondari. Walimu hao wanahudumia jumla ya shule 115, kati ya hizo 96 ni za msingi na 19 ni za Sekondari.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nanyumbu, Bw. Yohana Mrekoni akiendelea kutekeleza majukumu yake.

WAJUMBE WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAPOKEA RASIMU YA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA TUME KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025/2026 NA KUPOKEA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA (JULAI - DESEMBA)

Na Mwandishi Wetu- Morogoro

Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamepitia na kuipokea Rasimu ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida wa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, na kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha wa 2024/2025

Hatua hiyo ni sehemu ya taratibu za kupitisha mapendekezo ya bajeti kwa mujibu wa maelekezo ya Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na bajeti uliotolewa na Wizara ya fedha kwa mwaka 2025/26. Taasisi zinapaswa kupitisha mapendekezo ya bajeti kabla ya kufikishwa bungeni kwenye Bunge la Bajeti ya mwaka 2025/26 litakaloanza mwezi Aprili, 2025.

Akiwasilisha Rasmi hiyo yenye jumla ya shilingi bilioni 19 tarehe 17 Januari, 2025 mjini Morogoro kwenye kikao maalumu cha Mkutano wa Tume, Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, Bibi Evodia Pangani alisema, katika kutekeleza majukumu yake Tume ya Utumishi wa Walimu kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 imeainisha vipaumbele kuwa ni kusimamia utumishi wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo katika utumishi wa umma katika masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu; kuongeza uwezo wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika kutoa huduma kwa Walimu; na kuimarisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA hususan Mfumo TSCMIS katika kutoa huduma kwa Walimu.

Aliongeza kuwa vipaumbele vingine ni kufanya Utafiti na kutathmini kuhusu hali ya Walimu Nchini na kubainisha aina na mahitaji ya Walimu, idadi na ngazi ya Walimu wanaohitajika na kumshauri Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa na Waziri wa Elimu; kufanya mapitio ya utekelezaji wa Sheria Sura ya 448 na Muundo wa Tume ya Utumishi

wa Walimu; na kuanza kujenga Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume la Makao Makuu la Njedengwa Dodoma na kuanza ujenzi wa Ofisi 15 za Wilaya zenye hali mbaya.

Bibi Evodia aliongeza kuwa wanakusudia kuboresha utunzaji wa Kumbukumbu za Walimu kwa ajili ya maandalizi ya kuingiza taarifa hizo kwenye Mfumo wa TSCMIS, kununua vitendea kazi yakiwemo magari ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu.

Aidha aliongeza kuwa katika mwaka wa Fedha 2025/2026 Tume itaendelea na jukumu lake la msingi la kuhudumia walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, ambao hadi kufikia Desemba, 2024 walikuwa 273,736, kati yao Walimu wa Shule za Msingi ni 180,870 na Sekondari ni Walimu 92,886.

Awali akiwasilisha utekelezaji wa Bajeti na matumizi kwa mwaka 2024/ 2025 kwa kipindi cha nusu mwaka 2024/2025 kuanzia Julai hadi Desemba, 2024 kwa Wajumbe wa Tume, Mchumi Mkuu kutoka Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini Bw. Elia Malaki alisema kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024, Tume ilipokea jumla ya shilingi bilioni 10.8 toka Wizara ya Fedha sawa na asilimia 47 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/25

Alisema kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.1 ni kwa ajili ya mshahara, Shilingi bilioni 3.2 ni za Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yanayofadhiliwa na Mradi wa GPE - TSP, Shilingi milioni 327.5 kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Shilingi milioni 953.5 kwa ajili ya mradi wa BOOST.

Bw. Malaki alisema kuwa matumizi halisi hadi kufikia tarehe 15 Januari, 2025 yalikuwa ni shilingi bilioni 10 kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 5.1 ilikuwa ni kwa ajili ya mshahara, Shilingi bilioni 2.9 ni za Matumizi Mengineyo (OC), shilingi milioni 582.3 kwa ajili ya Mradi wa GPE - TSP na shilingi 327.5 kwa ajili



Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bibi Evodia Pangani akiwasilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 wakati wa kikao maalumu cha Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

ya Mradi wa BOOST.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke aliitaka Menejimenti ya Tume wakati wa kufanya utafiti kuhusu masuala ya Ustawi wa Walimu kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu na Watafiti kufanya utafiti utakaojibu changamoto mbalimbali zinazohusu Kada ya Ualimu nchini.

Alisema kuwa kabla ya kufanya utafiti ni vema wakaangalia tatizo ni nini na hapo ndipo wanaweza kushirikiana na Vyuo Vikuu kupata Wataalamu watakasaidia kupata majibu ambayo yataiwezesha Tume kumshauri Waziri wenye dhamana ipasavyo.

Prof. Muruke alisema kuwa kuhusu mpango wa kuanza kujenga Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya wilaya ambazo ziko katika hali mbaya, ni vema uende sambamba na kuwa na mpango wa ukarabati wa Ofisi ambazo zimechakaa ikiwemo kutenga Ofisi (Partition) kuruhusu mteja kuhudumiwa kwa uhuru na usiri.


**WAJUMBE WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAPOKEA
RASIMU YA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA
TUME KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025/2026 NA KUPOKEA
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2024/2025
KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA (JULAI - DESEMBA)**



Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bibi Evodia Pangani akiwasilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 wakati wa kikao maalumu cha Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu.



Mchumi Mkuu kutoka Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini Bw. Elia Malaki akiwasilisha utekelezaji wa Bajeti na matumizi kwa mwaka 2024/2025 kwa kipindi cha nusu mwaka 2024/2025 kuanzia Julai hadi Desemba, 2024 kwa Wajumbe wa Tume tarehe 17 Januari, 2025 mjini Morogoro.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiongoza kikao maalumu cha Wajumbe wa TSC cha kupia Rasimu ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa na Kushoto ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akitoa ufafanuzi wakati wa kikao maalumu cha Wajumbe wa Tume cha kupitia Rasimu ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026. Katikati ni Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke na Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Tume Bi. Bahati Mgongolwa.

WALIMU 807 WAPANDISHWA VYEO NDANI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NACHINGWEA

Na Mwandishi Wetu – Nachingwea.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepandisha vyeo jumla ya Walimu 807 wa Wilaya ya Nachingwea ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nachingwea, Bw. Tumaini Millanzi wakati wa mahojiano maalumu na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa kati ya walimu hao wa Shule za Msingi walikuwa 566, Sekondari 241 walikuwa 241 na kuongeza kuwa katika kipindi hicho ni walimu watatu (3) ndio waliosajiliwa ikiwa Shule ya Sekondari mawili (2) na Msingi mmoja (1).

Bw. Millanzi alisema kuwa katika kipindi hicho walimu 11 walibadishwa Cheo baada ya kujiendeleza kitaaluma ikiwa Sekondari ni mwalimu mmoja na walimu 10 ni kutoka Shule za Msingi.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024 walimu 55 walithibitishwa kazini ikiwa



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nachingwea, Bw. Tumaini Millanzi wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC ofisini kwake.

ni 27 kwa Shule za Msingi na walimu 28 kutoka Sekondari.

“Walimu wa Wilaya ya Nachingwea wanajivunia uongozi wa Awamu ya Sita unaoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutatua kero zao mbalimbali kama vile upandishwaji wa vyeo vya kawaida na mserereko pia uliopwaji wa stahiki mbalimbali ikiwemo mapunjo ya mishahara,” alisema.

Alisema kuwa kupitia Samia Mobile Clinic iliyofanyika katika Mkoa wa Lindi kuanzia tarehe 9 hadi 11 Januari, 2025 imesaidia kutambua madeni ya likizo, uhamisho, matibabu na mapunjo ya mishahara na Serikali kuendelea kulipa madeni hayo.

Alisema kuwa sanjari na hilo, Serikali ya Awamu ya Sita imewazesha kutoa mafunzo kwa Kamati za Wilaya ambayo yamewajengea uwezo wa kuamua mashauri kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu bila upendeleo wala kumuonea mtu.

Bw. Millanzi aliongeza kuwa Serikali kwa kutambua kuwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu ndio Mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu wametoa mafunzo kwao ambayo yamesaidia kurekebisha tabia za walimu kupitia mafunzo wanayowapa na kupunguza mashauri ya kinidhamu.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nachingwea, Bw. Tumaini Millanzi (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Nidhamu wa TSC, Bi. Yonila Chitanda (wa pili kutoka kulia), Afisa Ajira wa TSC, Bw. Louis Maluchila (wa pili kutoka kushoto) na Afisa Ajira wa TSC Bw. Hamisi Marwanga (kushoto) mara baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC Makao Makuu hivi karibuni.

MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI ZA TSC WILAYA YAONGEZA UFANISI KWA KAZI KWA KAMATI YA TSC MTWARA

Na Mwandishi wetu – Mtwara.

Mafunzo yaaliyoendeshwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwezi Septemba 2024 kwa Wajumbe wa Kamati za TSC ngazi Wilaya yamekuwa na matokeo chanya kutokana na utendaji kazi wa Kamati hizo kuonesha madabiliko katika utendaji wa kazi.

"Katika kikao cha mwisho kilichofanyika baada ya mafunzo tumeona tofauti kubwa katika kujenga hoja, kutafsiri Kanuni na kuzingatia zaidi taratibu za uendeshaji wa mashauri," hayo yamesemwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mtwara, Bw. Dankan Bushiri wakati akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC waliotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.

Bw. Bushiri alisema kuwa kwa sasa wajumbe wa Kamati katika Wilaya yake wamekuwa na uelewa mkubwa wa masuala ya Sheria na Kanuni zinazosimamia utumishi wa walimu pamoja na taratibu za uendeshaji wa mashauri ya walimu.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha nyuma vikao vilikuwa vinatumia muda mrefu kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya sheria kwa wajumbe hao na hivyo kufanya Katibu wa Kamati kutumia nguvu kubwa katika kutoa elimu na ushauri ili kufikia maamuzi yanayoendana na sheria.

"Kabla ya mafunzo kulikuwa na mivutano sana kwa wajumbe kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya sheria. Kila mmoja alikuwa anataka maamuzi yafanyike kwa namna anavyoona yeye bila kujua kwamba hata kama ni uamuzi/adhabu ni lazima iwe imetajwa kwenye Kanuni



zetu. Ilikuwa inatupa kazi ya ziada kutoa elimu na kushauri ili kufikia uamuzi," alisema Bw. Bushiri.

Alisema pamoja na Kamati hiyo kufanya vizuri kwenye vikao, wajumbe wake wameendelea kuwa mabalozi wazuri kwani wanaendelea kutoa elimu kwa walimu mbalimbali katika wilaya hiyo na hivyo kusaidia walimu kuzingatia taratibu katika masuala mbalimbali ya kiutumishi.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo, anaamini kuwa maamuzi ya mashauri ya walimu yatazingatia taratibu zote na haki itatendeka kwa mujibu wa Sheria Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na za Utumishi wa Umma.

Akizungumzia kuhusu mafunzo kwa wakuu wa shule za msingi, kiongozi huyo alisema mafunzo hayo yamesaidia walimu wakuu kujiamini na kutambua kuwa wao ni mamlaka ya kwanza ya Nidhamu kwa walimu hivyo wanapaswa kusimamia walimu kikamilifu.

"Baada ya mafunzo walimu wakuu wanatekeleza majumu yao kwa weledi na kujiamini, pale inapohitajika kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mwalimu unaona kweli taratibu zinazingatiwa," alisema Bw. Bushiri.

Bw. Bushiri alifafanua kuwa walimu wakuu waliopata mafunzo ni wa Halmashauri moja tu wakati Wilaya ya Mtwara inahudumia Halmashauri tatu (3) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara na Halmashauri ya Mji Nanyamba.

Hivyo, aliomba Menejimenti ya TSC kuona namna ya kuwapatia mafunzo walimu wakuu wote kwani mafunzo hayo yamekuwa na manufaa kwani yamesaidia kurahisisha utendaji wa kazi wa Tume na kufanya walimu kuzingatia taratibu zote za kiutumishi katika kutekeleza majukumu yao.



MENEJIMENTI YA TSC YATAKIWA KUPONGEZA WATUMISHI WANAOFANYA KAZI KWA BIDII

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke ameiagiza Menejimenti ya Tume hiyo kuhakikisha inatambua juhudi na kutoa pongezi kwa Watumishi wanaotekeleza majukumu yao kwa bidii.



Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu wakiimba wimbo wa 'Solidarity' kabla ya kuanza kwa mkutano wa Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.

Ametoa kauli hiyo tarehe 8 Janauri, 2025 wakati akizindua Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu lilofanyika katika Ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.

Prof. Muruke alisema kuwa ni vema Menejimenti wakaendelea kusimamia watumishi walio chini yao ili kuwa wabunifu, kutumia taaluma na ujuzi ili kuboresha utendaji kazi. Aliwataka kuhakikisha wanazingatia miongozo katika kuboresha mazingira ya kazi ikiwepo kuwapatia watumishi stahili zao na kufanya kazi kwa umoja, upendo na mshikamano ili kuleta tija kwa Tume na Taifa kwa ujumla.

Aidha, aliwakumbusha Wajumbe juu ya kuzingatia dhana ya haki na wajibu wao mahali pa kazi ili dhana hiyo itumike kutekeleza majukumu ya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Prof. Muruke aliitaka Menejimenti isisite kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Kuna Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma lakini hayo hayataweza kuleta tija bila ushirikiano kati ya mwajiri na watumishi," alisema Prof. Muruke.

Awali Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa Tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu lilikuwa na Baraza la Wafanyakazi ambalo lilifikia ukomo wake Septemba, 2023 kwa mujibu wa Mkataba wa awali.

Aidha, mchakato wa kuanzishwa kwa Baraza hilo umefanyika baada ya kukamilika kwa zoezi la kuhuisha Mkataba, uchaguzi wajumbe, wawakilishi na viongozi wapya wa Baraza la Wafanyakazi kwa nafasi ya Katibu na Katibu Msaidizi.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa Baraza hilo limeundwa kwa kuzingatia Muundo wa Mkataba wa Baraza ambao umeanza Oktoba, 2024 na utamalizika Oktoba, 2027.

Alisema kuwa baada ya kuzinduliwa kwa Baraza hilo kulikuwa na Wasilisho la Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume kwa Nusu Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Julai – Desemba, 2024 na Wasilisho la Rasimu ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

Mwl. Paulina aliwataka wajumbe kuwa mabalozi wema kwa kutoa mrejesho kwa watumishi wenzao juu ya yale yaliyojadiliwa katika Mkutano huo na kuongeza kuwa kwa kufanya hivyo watakuwa wameitenda haki nafasi yao na rasilimali zilizotumika kuendesha Mkutano huo.

Kabla ya kuzinduliwa kwa Baraza jipya Wajumbe walimchagua Mwl. Nuhu Mlekwa kuwa Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kupata kura 51 na Bi. Jenifer Maagi alipata kura 16 na kuwa Katibu Msaidizi.

MENEJIMENTI YA TSC YATAKIWA KUPONGEZA WATUMISHI WANAOFANYA KAZI KWA BIDII



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa Mkutano wa Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu ambaye pia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo ya awali kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi kwa ajili ya Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia alikuwa Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akitoa hotuba wakati wa Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.

MENEJIMENTI YA TSC YATAKIWA KUPONGEZA WATUMISHI WANAOFANYA KAZI KWA BIDII



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia alikuwa Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya TSC mara baada ya Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia alikuwa Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akiwa katika picha ya pamoja na Wawakilishi wa Baraza la Wafanyakazi kutoka kila Idara na Vitengo vya TSC mara baada ya Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia alikuwa Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akiwa katika picha ya pamoja na Wawakilishi wa Baraza la Wafanyakazi kutoka Kanda ya mara baada ya Uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 8 Januari, 2025 katika ukumbi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, jijini Dodoma.

WALIMU WILAYANI NEWALA WATAKIWA KURIDHIKA NA MAZINGIRA YA KAZI



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Newala, Bi. Asha Chambanda akizungumza na Maafisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC (harwapo pichani) hivi karibuni katika ofisi za Tume hiyo mjini Newala.

Na Mwandishi wetu – Newala.

Walimu wilayani Newala wametakiwa kuridhika na mazingira ya kazi na kutekeleza majukumu yao kwa kujituma huku wakizingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi ili kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa kikamilifu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Newala, Bi. Asha Chambanda wakati akizungumza na Maafisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC waliotembelea Ofisi za Tume Wilaya ya Newala kwa lengo la kupata habari za namna Tume hiyo inavyotoa huduma kwa Walimu.

Bi. Asha alieleza kuwa kumekuwa na tabia ya baadhi ya walimu wachache ambao hawataki kuridhika na mazingira ya kazi na hivyo kutumia muda mwingi kuzunguka kwenye ofisi za Serikali kufuatilia masuala ya uhamisho muda ambao wangepaswa kuwa darasani kufundisha.

Alisema hali hiyo inawanyima wanafunzi haki ya kufundishwa jambo ambao ni kinyume na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita

inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imekuwa ikifanya jitihada kubwa kuleta maendeleo katika sekta ya elimu.

Alisema kuwa katika kufuatilia masuala hayo ya uhamisho, baadhi ya walimu wanaondoka kwenye vituo vyao vya kazi bila kuomba ruhusa huku wengine wakichelewa kuripoti kwenye vituo vyao vya kazi baada ya muda wa likizo kumalizika na hivyo kusababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa kosa la utoro.

“Wapo baadhi ya walimu ambao unaona kabisa hawataki kubadilisha mitazamo yao na kuridhika na mazingira ya kazi ya huku. Unakuta Mwalimu siku ya kwanza tu anaripoti kazini lakini anaulizia taratibu za uhamisho. Wakienda kwenye vituo vya kazi siku mbili tatu unakuta wapo huku wilayani wanahangaika na masuala ya uhamisho. Hii inawanyima wanafunzi haki ya kupata elimu,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Aliongeza kuwa baadi ya walimu wamekwenda mbali zaidi na kujihusisha na masuala ya kughushi vibali vya uhamisho ili tu waweze kuhama jambo ambalo ni kinyume na taratibu za Utumishi wa Walimu na

zile za Utumishi wa Umma na hivyo kujikuta wakichukuliwa hatua za nidhamu.

Akizungumzia namna TSC Newala inavyokabiliana na changamoto hiyo, Bi. Asha alisema kuwa elimu imeendelea kutolewa kupitia mikutano katika ngazi ya Kata, Klasta, Shule na pale inapohitajika kukutana na Mwalimu mmoja mmoja kwa ajili ya kutoa ushauri kabla ya kufikia hatua ya kuchukua hatua za kinidhamu.

“Tunapokutana na walimu tunawaeleza kuhusu umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma na kuonesha madhara yanayoweza kutokea pale Mwalimu anapokwenda kinyume na taratibu hizo,” alisema Bi. Asha.

Katika kuongeza nguvu zaidi ya kutoa elimu, Bi. Asha aliomba Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kufanya utaratibu ili Walimu Wakuu katika Wilaya ya Newala waweze kupatiwa mafunzo kama ilivyofanyika kwa walimu wa Wilaya zingine.

“Nina amini wilaya ambazo Walimu Wakuu walipatiwa mafunzo, changamoto hizi za ukiukwaji wa maadili zimepungua sana. Hivyo, na mimi ninaomba ufanyike utaratibu ili walimu wa Wilaya hii nao waweze kupata mafunzo,” alihitimisha.

Wilaya ya Newala ni miongoni mwa Wilaya tano (5) zinazounda Mkoa wa Mtwara huku ikiwa na Halmashauri mbili (2) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Newala na Halmashauri ya Mji Newala.

Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina jumla ya Walimu 603 wanaohudumiwa na TSC, kati ya hao wa shule za msingi ni 417 na sekondari ni 186 huku ikiwa na shule 96 ambapo za msingi ni 78 na sekondari ni 18.

Kwa upande wa Halmashauri ya Mji Newala jumla ya walimu ni 456, kati ya hao walimu 306 ni wa shule za Msingi na 150 ni wa shule za Sekondari huku ikiwa na jumla ya shule 59 ambapo 46 ni za msingi na 13 ni za sekondari.

SERIKALI YAPANDISHA VYEO WALIMU 313 WA WILAYA YA LIWALE

Na Mwandishi Wetu – Liwale.

Serikali imepandisha vyeo jumla ya Walimu 313 wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 kati yao walimu hao kutoka Shule za Msingi ni 193 na Sekondari ni walimu 120.

Kauli hiyo imetolewa hivi karinuni na Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Liwale, Bw. Julius Linje wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC ofisini kwake.

Alisema kuwa TSC Wilayani Liwale inahudumia jumla ya walimu 586 kati yao wa Shule za Msingi ni 370 na Shule za Sekondari ni 216.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho jumla ya walimu 52 ambapo wa Shule za Msingi walikuwa 35 na Sekondari 17 walisajiliwa na

kuthibitishwa kazini.

Aidha, Bw. Linje alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu wilayani humo inafanya ziara katika shule mbalimbali na kuendesha vikao na walimu wakuu na Wakuu wa Shule, kufanya vikao na walimu wapya kazini na kugawa vipeperushi na vijitabu kwa ajili ya kuwaelimisha walimu wasiilingie katika kukikuka maadili ya kazi ya ualimu.

Alisema kuwa hatua hiyo imesaidia kupunguza makosa ya kimaadili na walimu wakuu na wakuu wa shule wameweza kusimamia majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Katika hatua nyingine TSC Wilaya ya Liwale inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada mbalimbali inayoendelea kuzifanya ikiwemo upandishaji walimu vyeo kwa wakati na kuondoa changamoto ya walimu waliokaa kwenye cheo kimoja kwa



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Liwale, Bw. Julius Linje akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC hivi karibuni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume.

muda mrefu.

Bw. Linje alisema kuwa pia Serikaili imejitahidi kulipa madeni ya walimu, imeongeza idadi ya walimu wa ajira mpya ambao wamesaidia kupunguza uhaba wa walimu na imiweka miundombinu ya nyumba za walimu, madarasa katika Shule za Msingi na Sekondari.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Liwale, Bw. Julius Linje ((katikati)) akiwa katika picha ya pamoja na maafisa katika ofisi hiyo Bw. Abdulrahim Kindimbo (kushoto) na Bi. Masha Mpoto (katikati) mara baada ya kumalizika kwa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC hivi karibuni wilayani Liwale.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Liwale, Bw. Julius Linje (kulia) akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC hivi karibuni wilayani Liwale. Wengine katika picha ni Maafisa wa TSC Wilaya ya Liwale, Bw. Abdulrahim Kindimbo (kushoto) na Bi. Masha Mpoto (katikati)

TSC YAKUTANISHA WADAU KUTOA MAONI KATIKA KUANDAA MWONGOZO WA MAFUNZO YA USIMAMIZI WA MASUALA YA NIDHAMU NA RUFAA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeandaa kikao kazi kinachowakutanisha wadau wa elimu kwa lengo la kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa umma.

Akifungua kikao hicho tarehe 15 Januari, 2025 mjini Morogoro, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke alisema lengo la Tume kuandaa Mwongozo huo ni kuwajengea uwezo watumishi wa Tume, Mamlaka za nidhamu na Wajumbe wa Tume kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu.

Prof. Muruke aliwataka wadau kutoa maoni kwa uhuru na weledi ili kuweza kuandaa mwongozo utakaosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa mamlaka za Nidhamu na rufaa kwa walimu.

Aliongeza kuwa katika kuandaa mwongozo huo ushiriki wa wadau mbalimbali wa elimu ni jambo muhimu ili kuhakikisha mambo yote muhimu yanazingatiwa.

Aidha, Mwenyekiti huyo alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za dhati za kuiwezesha Tume kuwa sehemu ya mikakati ya Taifa katika kuinua kiwango cha elimu na kusimamia mazingira ya kazi ya walimu ili kuinua kiwango cha elimu kupitia ufundishaji na ujifunzaji.

"Natambua kwamba kuwepo kwetu hapa ni matokeo ya juhudi za Serikali anayoiongoza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kupitia ufadhili kutoka Global Partnership for Education (GPE), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikishirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, inatekeleza Programu ya

miaka minne (2023/24 hadi 2026/27) ya Uboreshaji wa Kada ya Ualimu (Teacher Support Programme - TSP)," alisisitiza.

Awaliakitoa maelezo ya utangulizi, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, inatekeleza Programu ya miaka minne (2023/24 hadi 2026/27) ya Uboreshaji wa Kada ya Ualimu (Teacher Support Programme - TSP).

Alisema kuwa lengo kuu la programu hiyo ni kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ili kuinua kiwango cha elimu nchini.

Mwl. Paulina alisema kuwa katika utekelezaji wa programu hiyo, Tume ya Utumishi wa Walimu ina jukumu la kutoa mafunzo kwa watumishi wa Tume na Makamishna kuhusu

uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu.

Alisema kuwa kwa msingi huo, Tume ya Utumishi wa Walimu kupitia programu ya Uboreshaji wa Kada ya Ualimu (Teacher Support Programme - TSP) chini ya mradi wa Global Partnership for Education (GPE), imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma utakaoziwezesha mamlaka za nidhamu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mwl. Paulina alisema mara baada baada ya mwongozo huo kukamilika mafunzo yatatolewa kwa wadau mbalimbali wanaohusika na usimamizi wa masuala ya nidhamu na rufaa za walimu ili kuwaongezea uelewa katika sheria, kanuni, na taratibu zinazotumika katika kuendesha masuala hayo.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa hotuba ya kufungua kikao kazi cha wadau wa elimu kwa ajili ya kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 15 Januari 2025 mjini Morogoro.

TSC YAKUTANISHA WADAU KUTOA MAONI KATIKA KUANDAA MWONGOZO WA MAFUNZO YA USIMAMIZI WA MASUALA YA NIDHAMU NA RUFAA KWA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa tarehe 21 Januari, 2025.

Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Fatuma Muya akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi cha wadau wa elimu kwa ajili ya kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 15 Januari 2025 mjini Morogoro.



Mshiriki wa Kikao kazi cha kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma ambaye pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Lazaro Komba akitoa maoni yake wakati wa kikao hicho tarehe 15 Januari 2025 mjini Morogoro.

Mshiriki wa kikao kazi cha kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa umma ambaye pia aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Christina Hape akitoa maoni yake wakati wa kikao hicho tarehe 15 Januari 2025 mjini Morogoro.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (Katikati waliokaa) akirwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC mstaafu, Prof. Willy Komba (wa tatu kutoka kushoto), aliyewahi kuwa Katibu Tarwala ambaye kwa sasa ni mtumishi wa umma mstaafu, Mwl. Bernard Makali, aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Christina Hape (wa pili kutoka kulia) na baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 15 Januari mjini Morogoro.

TSC YAKUTANISHA WADAU KUTOA MAONI KATIKA KUANDAA MWONGOZO WA MAFUNZO YA USIMAMIZI WA MASUALA YA NIDHAMU NA RUFAA KWA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (Katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa kikao kazi cha kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 15 Januari mjini Morogoro.



Washiriki wa kikao kazi cha kutoa maoni ya Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma wakiwa katika kikao kazi hicho tarehe 15 Januari mjini Morogoro.

WALIMU TANDAHIMBA NA MATUMAINI YA KUTATULIWA KERO ZAO CHINI YA UONGOZI WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Tandahimba, Bw. Chihako Mohamed akitoa maelezo kuhusu ofisi hiyo inavyowahudumia walimu wa Wilaya ya Tandahimba hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Tandahimba.

Walimu Wilayani Tandahimba wana matumaini makubwa kuwa chini ya ongozi wa Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan maslahi yao yataendelea kuboreshwa ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Hayo yamebainishwa na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tandahimba, Bw. Chihako Mohamed wakati akizungumza na Maafisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC waliotembelea ofisi hiyo hivi karibuni kwa lengo la kupata habari za namna ofisi hiyo inavyohudumia walimu.

Bw. Mohamed alisema matumaini hayo ya walimu yanatokana na namna Serikali inavyoshughulikia kero na malalamiko yao mbalimbali jambo ambalo limeongeza morali ya utendaji wa kazi na hivyo kuinua kiwango cha elimu.

Alisema moja ya changamoto za walimu ni madeni ya fedha za uhamisho, likizo na malimbikizo ya mishara ambayo kwa kiasi kikubwa yamelipwa na bado yanaendelea kulipwa hivyo hatua hiyo ya Serikali imeendelea kuwaongezea walimu ari ya utendaji wa kazi.

“Hivi karibuni imeendeshwa kliniki ya kushughulikia kero na changamoto

mbalimbali za walimu. Sisi TSC kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali tulifanikiwa kuwafikia walimu wengi na kero nyingi zilitatuliwa papo kwa papo. Hivyo, walimu wengi wameongeza matumani na Rais Samia baada kuona yale waliyokuwa wanayapigia kelele kwa miaka mingi sasa yanatatuliwa bila vikwazo,” alisema Bw. Mohamed.

Pamoja na Hayo, Bw. Mohamed aliwakumbusha walimu kuacha tabia za uzembe na kutojali wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu iliyokusudiwa.

Vilevile, Afisa huyo aliwataka walimu wa Wilaya hiyo kuridhika na mazingira ya kazi na kuachana na tabia ya kutumia muda wa kazi

kushughulikia masuala ya uhamisho badala ya kutulia shuleni na kufundisha wanafunzi.

“Tunatambua kwamba uhamisho ni haki ya mtumishi, lakini ili kupata haki hiyo ni lazima sheria, kanuni na taratibu zizingatiwe. Ninawasihi walimu kuacha kutumia njia za mkato katika kushughulikia masuala ya uhamisho jambo ambalo linafanya baadhi yao kughushi vibali vya uhamisho na kusababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu,” alisema Bw. Mohamed.

Akizungumzia juu ya mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Msingi yaliyotolewa mwaka 2024, Bw. Mohamed alisema kuwa yamesaidia kufikisha elimu kwa walimu wengi shuleni kwani kila mkuu wa shule alitakiwa kutoa mafunzo hayo kwa walimu anaowasimamia.

“Kutokana na uelewa huo, tunaamini walimu wataendelea kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazotakiwa. Hivyo, hata utendaji wa makosa tunaona unapungua kwa kiasi kikubwa huku utendaji kazi na uwajibikaji vikiendelea kuongezeka,” alisema.

Wilaya ya Tandahimba ina jumla ya shule 163 za Serikali ambapo katika idadi hiyo shule za msingi ni 131 na shule za sekondari ni 32 huku ikiwa na jumla ya walimu 1320 waohudumiwa na TSC ambapo walimu 927 ni wa shule za Msingi na 393 ni wa shule za sekondari.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Tandahimba, Bw. Chihako Mohamed akiendelea kutekeleza majukumu yake ofisini kwake.

TSC KILWA YAISHUKURU SERIKALI KWA KUWAWEZESHA KUTOA MAFUNZO KWA KAMATI YA WILAYA

Na Mwandishi Wetu – Kilwa.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi imeishukuru Serikali kwa uwezesaji uliowasaidia kutoa mafunzo ya kujengea uwezo Kamati yao ili iweze kutekeleza majukumu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu inaposhughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 27



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa, Bw. Omari Mkuwili akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC ofisini kwake kuhusu mafanikio ya utekelezaji majukumu.



Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa Bi. Somoe Makokola akiendelea na utekelezaji wa majukumu yake



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa, Bw. Omari Mkuwili (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Ajira wa TSC Wilaya ya Kilwa Bi. Somoe Makokola (kulia) mara baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC Makao Makuu hivi karibuni.

Januari, 2025 na Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa, Bw. Omari Mkuwili wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC ofisini kwake.

Alisema kuwa mafunzo kwa wanakamati wa Wilaya ya Kilwa yamesaidia kupanua uelewa wa kuchambua, kuhoji vifungu vya kisheria vinavyoambatana na utoaji wa maamuzi katika mashauri ya walimu yanayowasilishwa kwao.

“Wilaya ya Kilwa tunajivunia sana uongozi wa awamu sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha kuapata vitendea kazi ambavyo vinasaidia kutoa huduma bora kwa walimu kwa wakati ikiwemo kutoa barua za kuwathibitisha kazini na kupandishwa vyeo,” alisema.

Bw. Mkuwili alisema kuwa kwa upande wa Walimu wa Wilaya ya Kilwa wanajivunia uwepo wa uongozi wa Awamu ya Sita kwa namna unavyoshughulikia masuala yao ikiwemo kwa kuhakikisha kuwa kila Mwalimu anakuwa katika sehemu yake kulingana na umri kazini na kiwango cha elimu.

Alisema kuwa katika mwaka wa

fedha wa 2023/2024 walimu 598 walipandishwa vyeo ikiwa kwa shule za Msingi walikuwa ni 414 na Sekondari 184 na kuongeza kuwa katika kipindi hicho walimu waliosajiliwa na kuthibitishwa kazini walikuwa 94.

Bw. Mkuwili aliongeza kuwa Rais Samia yuko mstari wa mbele katika kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia kama vile madarasa, nyumba za walimu na ruzuku za elimu bure kufika kwa wakati.

Aidha, alisema kuwa Wilaya ya Kilwa imendelea kushughulikia madaai ya walimu yanayotokana na likizo, matibabu, uhamisho kwa utaratibu wa kulipa aliyetangua kisha anayefuata (first in -first out).

Katika hatua nyingine, Mkuwili alisema kuwa TSC imekuwa ikendelea na ziara katika shule mbalimbali kwa ajili ya utoaji wa elimu kwa walimu kupitia mikutano, vipeperushi ili kuwajengea uwezo wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao.

Alitaja changamoto zinazowasababisha baadhi ya walimu kujikuta wakikiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wao ni pamoja na ulevi, utoro na ukaidi.

TSC RUANGWA YAPONGEZA JUHUDI ZA RAIS SAMIA KATIKA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Ruangwa.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ruangwa imempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutatua changamoto mbalimbali za walimu na hivyo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa moyo.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Afisa Nidhamu wa TSC Wilaya ya Ruangwa, Bw. Yahya Mnaide wakati wa mohojiano maalumu na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa moja wapo ya changamoto iliyokuwa ikiwakabili walimu ilikuwa kutopandishwa Madaraja ambapo katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, jumla ya walimu 538 walipandishwa ikiwa wa Shule za Msingi walikuwa 322 na Sekondari 216.

Bw. Mnaide alisema kuwa katika mwaka huo wa fedha jumla ya walimu 56 walisajiliwa ambapo wa shule za Msingi walikuwa 36 na Sekondari 20 na kuongeza kuwa walimu 30 kutoka Sekondari walithibitishwa kazini.

Aliongeza kuwa walimu wanajivunia Uongozi wa Rais Samia kwa kuwalipa mapunjo ya mishahara na madeni ya likizo kwa wakati.

“Ofisi ya TSC Wilaya ya Ruangwa inaushukuru Uongozi wa Awamu ya Sita kwa kutatua changamoto ya madaraja kwa walimu pia kwa kuiwezesha Ofisi ya Tume kupata gari ambalo linatusaidia kutembelea Shule mbalimbali kwa ajili kutoa elimu kwa walimu,” alisema.

Bw. Mnaide alisema kuwa usafiri huo umewasaidia kuwafikia walimu kwa haraka na kuwapunguzia usumbufu wa kufika wilayani kwa ajili ya kuwapa elimu juu ya kanununi za maadili ya kazi ya ualimu ili kuwakinga wasijiingiza makosa yanayoharibu haiba ya ualimu.

Alisema kuwa sanjari na hilo, Serikali ya Awamu ya Sita imewazesha kutoa mafunzo kwa Kamati za Wilaya ambayo yamewajengea uwezo wa kuamua mashauri kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu bila upendeleo

wala kumuonea mtu.

Bw. Mnaide aliongeza kuwa Serikali kwa kutambua kuwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu ndio Mamlaka ya kwanza ya nidhamu wametoa mafunzo kwao ambayo yamesaidia kurekebisha tabia za walimu kupitia mafunzo wanayowapa.

Katibu Msaidizi huyo wa TSC Wilaya

ya Ruangwa alisema kuwa pamoja juhudi zote wapo walimu ambao wanakiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi ya ualimu.

Alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya mashauri tisa (9) yalipokelewa yakiwemo matatu kutoka kwa walimu wa Shule za Msingi na Sita Sekondari.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ruangwa, Bw. Yahya Mnaide akizungumza hivi karibuni na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu juu ya juhudi za Serikali katika utatuzi wa changamoto za walimu.

RAIS SAMIA AMELETA FARAJA KWA WALIMU WILAYANI LINDI - TSC

Na Mwandishi Wetu-Lindi

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lindi imesema uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu umeleta Faraja kwa walimu wa Wilaya Lindi mara baada ya kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Afisa Nidhamu wa TSC Wilaya ya Lindi, Bw. Mohamed Said wakati wa mohojiano maalumu na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa uongozi wa Awamu ya Sita umesaidia kurudisha matumaini kwa walimu baada ya kupandisha vyeo na kuanza kulipa madeni yao ikiwemo ya mapunjo ya mishahara na uhamisho na hivyo kuwaongezea ari ya kufanyakazi na kuwa na mazingira tulivu ya kufanyia kazi.

Bw. Said alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inahudumia Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Mtama ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imepandisha vyeo jumla ya walimu 661.

Alisema kuwa katika Manispaa ya Lindi walipandishwa walimu 263 na Mtama walikuwa ni 398 na kuongeza kuwa katika kipindi hicho walimu 118 walisajiliwa na



Afisa Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lindi Bw. Mohamed Said akiwa katika mohojiano maalumu na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali wa Tume ya Utumishi wa Walimu hivi karibuni.

kuthibitishwa kazini.

Kwa upande wa Afisa Ajira wa TSC Wilaya ya Lindi Bw. Idrisa Mtivila aliishukuru Serikali kwa kuwawezesha kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati ya Wilaya na Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule ambayo yameleta matokeo chanya wakati wa kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu.

Alisema kuwa hatua hiyo imesaidia kupungua kwa mashauri baada elimu waliyopata kupelekwa kwa walimu wanaowasimbia ili waweze kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao kwa ajili ya kulinda haiba ya Mwalimu.

Bw. Mtivila alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imesaidia kuleta ustawi wa maadili, nidhamu kwa walimu kutokana na huduma bora ya kupatiwa stahili mbalimbali za kiutumishi ikiwemo za upandishwaji vyeo, kubadilishwa miundo ya kiutumishi na kulipwa kwa madai mbalimbali wanayodai.

Alisema kuwa baada ya kuundwa kwa Kamati ya kuhakiki madeni ya walimu zoezi linaendelea vizuri kutokana na mipango ni mikakati mbalimbali iliyowekwa.



Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lindi, Bw. Idrisa Mtivila akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali wa Tume ya Utumishi wa Walimu hivi karibuni kuhusu mafanikio ya TSC wilayani humo.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu